

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA



WITO WA KUTOA MAONI KUHUSU SHERIA YA KULINDA TAARIFA BINAFSI

1.0 Utangulizi

Licha ya masharti ya Ibara ya 16(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Sura ya 2, Tanzania inazo Sheria mbalimbali zinazolinda Taarifa Binafsi. Katika utekelezaji wa Sheria hizo, hasa kipindi hiki cha maendeleo makubwa katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Serikali na taasisi zake zimebaini upungufu ambao ni kikwazo katika hifadhi ya taarifa binafsi. Moja ya upungufu ni baadhi ya masharti ya Sheria hizo kugongana na kushindwa kuleta ufanisi katika utekelezaji wake. Kwa kutambua upungufu huo, Serikali, kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, inafanya utafiti ili kupata maoni na mapendekezo kutoka kwa wananchi na wadau kwa lengo kutunga Sheria mahsusi ya kuhifadhi taarifa binafsi.

2.0 Madhumuni ya Utafiti

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania. Tume na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, zinafanya utafiti wa mfumo wa Sheria ya Kulinda Taarifa Binafsi kwa lengo la:

- (i) Kuangalia hali halisi ya utekelezaji wa sheria zilizopo;
- (ii) Maoni kuhusiana na sheria inayopendekezwa;
- (iii) Udhaifu katika masharti ya Sheria zilizopo;
- (iv) Maeneo ya sheria yatakayoathirika kutokana na mapendekezo ya kutungwa Sheria ya Kulinda Taarifa Binafsi;
- (v) Sheria zitakazohitaji kuhuishwa ili kuondoa mgongano kwa lengo la kwenda sambamba na Sera ya Taifa ya Teknolojia na Habari; na
- (vi) Uundwaji wa Idara inayojitegemea ndani ya Mamlaka ya Mawasiliano itakayosimamia ulinzi wa taarifa binafsi.

3.0 Maoni na Mapendekezo ya Wananchi na Wadau

Ili kuwezesha kukamilika kwa utafiti huu na kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 10(1) (2) cha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Sura ya 171, Tume inatoa wito kwa watu binafsi, taasisi za Serikali na binafsi kushiriki katika kutoa maoni na mapendekezo kuhusu masuala au masharti yatakayopaswa kuzingatiwa katika Sheria ya Kulinda Taarifa Binafsi.

4.0 Muda wa Kupata Maoni/Mapendekezo

Kwa lengo la kukamilisha Utafiti huu mapema, Tume imeweka muda wa siku kumi na sita kuanzia tarehe 15 Agosti, 2016 hadi tarehe 31 Agosti, 2016 wa kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa Wananchi na Wadau kwa ujumla.

5.0 Namna ya Kutuma Maoni/Mapendekezo

Maoni na Mapendekezo yanaweza kuwasilishwa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania kupitia njia zifuatazo:

Anuani ya barua:

Katibu Mtendaji,
Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania,
S.L.P. 3580,
DAR ES SALAAM.

Simu ya Mezani:

Simu: +255 22 2123533/2111387

Nukushi:

Fax: 255 22 2123534

Barua pepe:

lrct@lrct.go.tz


Mtandao wa Kijamii:

www.facebook.com/tumesheria.tanzania

Tovuti:

www.lrct.go.tz

Imetolewa na:


Casmir S. Kyuki
KATIBU WA TUME